

# NI UPI USIKU WA LAYLATUL QADR

Swahili

Imeandikwa na:

Daudi Abubakari

: Imepitiwa na

Abubakari Shabani Rukonkwa





# ما هي ليلة القدر؟

السواحلية

**كتبه: دود أبوبكر**

المراجع:

**أبوبكر شعبان روكونكوا**



بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Utangulizi:

Hadiyth kadhaa zimetaja kuhusu usiku wa Laylatul-Qadr. Imetajwa kuwa ni katika masiku kumi ya mwisho; siku ya ishirini na moja, au ishirini na tatu, au ishirini na tano au ishirini na saba kwa dalili zifuatazo:

عن عائشة أن رسول الله صلى الله عليه وسلم قال: ((تحروا ليلة القدر في الوتر من العشر الأواخر)) رواه البخاري

Hadiyth ya 'Aiashah (Radhiya Allaahu 'anhaa) kwamba Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema: ((Utafuteni usiku wa Laylatul-Qadr katika siku za witiri kwenye siku kumi za mwisho)) [Al-Bukhaariy]

حديث ابن عباس رضي الله عنهما أن النبي صلى الله عليه وسلم قال: ((التمسوها في العشر الأواخر من رمضان ليلة القدر في تاسعة تبقى ، في سابعة تبقى ، في خامسة تبقى)) رواه البخاري

Hadiyth ya Ibn 'Abbaas (Radhiya Allaahu 'anhumaa) kwamba Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema: ((Utafuteni usiku wa Laylatul-Qadr katika siku kumi za mwisho za Ramadhaan; katika (usiku wa) tisa, saba, na wa tano utakaobakia [mwisho wa Ramadhaan])) [al-Bukhaariy]

Imaam Ahmad amepokea kutoka kwa 'Ubaydah bin As-Swaamit kwamba alimuuliza Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) kuhusu usiku wa Laylatul-Qadr akasema:

((فِي رَمَضَانَ فَالْتَمِسُوهَا فِي الْعَشْرِ الْاَوْاخِرِ فَاِنَّهَا فِي وَتُرِ اِحْدَى وَ عِشْرِينَ اَوْ ثَلَاثَ وَ عِشْرِينَ اَوْ خَمْسَ وَ عِشْرِينَ اَوْ سَبْعَ وَ عِشْرِينَ اَوْ تِسْعَ وَ عِشْرِينَ اَوْ فِي اٰخِرِ لَيْلَةٍ))



(( Katika Ramadhaan, utafuteni siku kumi za mwisho, hakika umo katika siku za witiri; siku ya ishirini na moja, au ishirini na tatu, au ishirini na tano, au ishirini na saba, au ishirini na tisa, au usiku wa mwisho)) [Ahmad]

Alama Zinazobainisha Laylatul-Qadr:

1. Usiku huo unakuwa na mwanga zaidi.
- 2 . Upepo siku hiyo hutulia, yaani siku hiyo hautokei upepo mkali.
3. Hali ya hewa huwa nzuri.
- 4 . Nyoyo za Waumini usiku huo huwa zina utulivu kuliko siku nyingine.
- 5 . Baadhi ya watu wema huoteshwa usiku huo kama walivyokuwa wakioteshwa Maswahaba na Salafus-Swaalih (wema waliotangulia)

Asubuhi Yake:

حديث أبي بن كعب رضي الله عنه أنه قال: "أخبرنا رسول الله صلى الله عليه وسلم أنها تطلع يومئذٍ لا شعاع لها" رواه مسلم



Hadiyth ya 'Ubay bin Ka'ab (Radhiya Allaahu 'anhu) kwamba: "Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) ametuambia kuwa, jua siku hiyo hutoka likiwa halina mishale (mikali)" [Muslim]

Pia:

ليلة القدر ليلة طلقة لا حارة ولا باردة ، تُصبح الشمس يومها  
حمرًا ضعيفًا)) صحيح ابن خزيمة

(( Laylatul-Qadr ni usiku ulio katika hali ya ukunjufu, usio na baridi wala joto, asubuhi yake jua huwa jekundu na dhaifu)) [Swahiyh Ibn Khuzaymah]

ليلة القدر ليلة بلجة (أي مضيئة) لا حارة ولا باردة ، لا يرمى  
فيها بنجم)) (أي لا ترسل فيها الشهب) رواه الطبراني ومسنده أحمد

((Laylatul-Qadr usiku wa kung'aa [yaani wenye mwanga] sio joto wala baridi, na vimondo



(nyota za kufyatuliwa) havitotumwa)) [At-Twabaraaniy na Ahmad[

Tunamuomba Allaah (Subhaanahu wa Ta'aalaa) Atuwezeshe kukesha masiku kumi ya Ramadhaan ili tujaaliwe kuupata usiku huu mtukufu, tutoke katika Ramadhaan tukiwa tumeghufuriwa madhambi yetu yote. Aamiyn

